JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA NISHATI
MAMLAKA YA UDHIBITI WA
HUDUMA ZA NISHATI NA MAJI
(EWURA)

ewura
Energy and Water Utilities Regulatory Authority
ISO 9001: 2015 Certified




# MUHTASARI WA TAARIFA YA UTENDAJI WA SEKTA NDOGO YA UMEME KWA MWAKA WA FEDHA 2024/25






JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA NISHATI
MAMLAKA YA UDHIBITI WA
HUDUMA ZA NISHATI NA MAJI
(EWURA)

ewura
Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji
ISO 9001:2015 Certified

# MUHTASARI WA TAARIFA YA UTENDAJI WA SEKTA NDOGO YA UMEME KWA MWAKA WA FEDHA 2024/25

MACHI, 2026

# YALIYOMO

UJUMBE WA MWENYEKITI WA BODI ........................................ iv
DIBAJI ........................................................................................ v
VIFUPISHO VYA MANENO ............................................................ vii
MUHTASARI WA RIPOTI................................................................ viii

1.0 UTANGULIZI................................................................................ 1

2.0 MUUNDO WA SEKTA NDOGO YA UMEME .................................... 2

3.0 LESENI NA USAJILI ..................................................................... 3

4.0 VIBALI VYA UJENZI WA VITUO VYA KUZALISHA UMEME........... 4

5.0 MIKATABA YA KUUZIANA UMEME ............................................. 4

6.0 BEI ZA KUUZA UMEME................................................................ 5

7.0 MALALAMIKO NA USULUHISHI .................................................. 5

8.0 UZALISHAJI WA UMEME.............................................................. 6
- 8.1 Uwezo wa mitambo ya kuzalisha umeme ................................ 6
- 8.2 Mahitaji ya Umeme..................................................................... 6
- 8.3 Mgawanyiko wa Uzalishaji wa Umeme ..................................... 7
- 8.4 Uzalishaji na Uingizaji Umeme toka Nchi Jirani ........................ 8

9.0 USAFIRISHAJI UMEME.................................................................. 8
- 9.1 Miundombinu ............................................................................... 8
- 9.2 Wateja ......................................................................................... 9
- 9.3 Ufanisi wa Miundombinu ............................................................. 9

10.0 USAMBAZAJI UMEME ................................................................ 10
- 10.1 Miundombinu.............................................................................. 10
- 10.2 Wateja ........................................................................................11
- 10.3 Ufanisi wa Miundombinu ........................................................... 12

11.0 UPOTEVU WA UMEME................................................................ 13

12.0 UWEKEZAJI KWENYE MIUNDOMBINU YA UMEME.................... 13
12.1 Uwekezaji katika miundombinu ya kuzalisha umeme...................... 13
12.2 Uwekezaji Katika Miundombinu ya Kusafirisha Umeme.................. 14
12.3 Ushiriki wa wawakezaji binafsi katika miundombinu ya umeme ...... 14

13.0 NISHATI SAFI YA KUPIKIA ........ 15

14.0 TATHMINI YA USHINDANI KATIKA SOKO ........ 15

15.0 MATOKEO YA UDHIBITI ........ 16

16.0 USIMAMIZI WA MASLAHI YA WATEJA ........ 17

17.0 MUONEKANO WA SEKTA NDOGO YA UMEME KATIKA MIAKA IJAYO ........ 18

18.0 MAFANIKIO ........ 18

19.0 CHANGAMOTO ........ 21

# UJUMBE WA MWENYEKITI WA BODI

**Kwa niaba ya Bodi ya Wakurugenzi ya Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), nina furaha kuwasilisha Taarifa ya Utendaji wa sekta ndogo ya umeme kwa Mwaka wa Fedha 2024/25.**

**Mojawapo ya malengo ya kimkakati ya EWURA ni kuhakikisha upatikanaji wa uhakika wa huduma ya umeme na wenye bei stahimilivu. Hii ni kwa sababu kutokana na kuwa umeme ni miongoni mwa vichocheo vikuu vya kukuza uchumi, kupitia uzalishaji viwandani na pia kutoa fursa nishati safi ya kupikia.**

**EWURA inaipongeza serikali kwa uwekezaji katika sekta ndogo ya umeme, ukiwemo mradi wa kuzalisha umeme wa megawati 2,115 wa bwawa la Julius Nyerere. EWURA inaipongeza pia sekta binafsi kwa uwekezaji. Juhudi hizi zimechangia kuhakikisha upatikanaji wa umeme na maendeleo ya kiuchumi na kijamii nchini.**

**Katika Mwaka wa Fedha 2024/2025, sekta ndogo ya umeme ilipata mafanikio mbalimbali. Miongoni mwa mafanikio hayo ni kuongezeka kwa wananchi wanaopata huduma ya umeme, miundombinu, uwekezaji, ufanisi wa utendaji wa kampuni za umeme, na uhakika wa kupatikana umeme.**

**Kwa heshima, napenda kuushukuru uongozi wa Wizara ya Nishati na Wizara ya Maji, kwa miongozo mbalimbali waliotupatia. Nawashukuru pia wadau wengine katika sekta ndogo ya umeme kwa ushirikiano wao. Tunawahakikishia kwamba EWURA itaendelea kutoa huduma za kiudhibiti za kiwango cha kimataifa kwa uwazi, uwajibikaji na uhodari.**

**Mwisho napenda kuishukuru Bodi ya EWURA, Menejimenti na wafanyakazi kwa ushirikiano na kuwezesha kukamilika kwa taarifa hii.**

Prof. Mark J. Mwandosya
**Mwenyekiti wa Bodi**

# DIBAJI

Kwa miaka nane mfululizo, Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) imekuwa ikiandaa taarifa za mwaka za utendaji wa taasisi zinazodhibitiwa Tanzania bara. Madhumuni ya taarifa hizo ni kuujulisha umma kuhusu hatua zilizofikiwa na taasisi hizo katika kutoa huduma ya umeme, kupima jitihada za taasisi hizo katika kufikia malengo yao na kupendekeza hatua za kuboresha utoaji wa huduma.

Taarifa hii inahusisha kampuni 37 zenye leseni za uzalishaji wa umeme, kampuni moja yenye leseni ya usafirishaji umeme na kampuni mbili zenye leseni za usambazaji umeme. Taarifa inahusisha pia kampuni 13 zilizosajiliwa kuzalisha au kusambaza umeme chini ya megawati moja hasa katika maeneo ambayo hayajafikiwa na gridi ya taifa. Taarifa pia inaeleza faida za utendaji wa leseni 10,367 za wafungaji wa mifumo ya umeme.

Kwa ujumla, utendaji wa taasisi zinazodhibitiwa unaendelea kuimarika na hivyo kuchangia katika mafanikio ya ukuaji wa sekta ndogo ya umeme. Mafanikio hayo ni pamoja na kuongezeka kwa uwezo wa mitambo ya kuzalisha umeme, kufikia MW 4,504.54 kutoka MW 2,411.33 Juni 2024, wakati ambapo mahitaji ya umeme yameongezeka kufikia MW 2,358.54 kutoka 1,654.2MW katika kipindi hicho.

Mafanikio mengine ni kuongezeka kwa miundombinu ya kusafirisha umeme kufikia km 8,303.87 kutoka km 7,524 Juni 2024, miundombinu ya usambazaji umeme kufika km 214,343.67 kutoka 188,266.23 Juni 2024, kuongezeka kwa wateja waliounganishiwa umeme kufikia 5,485,676 kutoka 4,982,259 Juni 2024.

Uwekezaji pia umeongezeka, ambapo miradi mbalimbali ipo katika hatua za kukamilika. Uwekezaji huo unahusisha miradi inayojengwa na serikali ikiwemo miradi mitano ya kuzalisha umeme wa jumla ya megawati 2,235.5, miradi 30 yenye kilomita 15,034.63 za miundombinu ya kusafirisha umeme, na miradi 33 ya vituo vya kupozea umeme. Uwekezaji kutokana na sekta binafsi nao uliongezeka kwa miradi 44 ya kuzalisha umeme wa megawati 209.62 na ambayo ilikuwa katika hatua mbalimbali za utekelezaji.

**Mafanikio haya yameweza kupatikana kutokana na mazingira wezeshi ya uwekezaji kwa kuratibiwa na Wizara ya Nishati kwa kushirikiana na TANESCO, taasisi zinazodhibitiwa, washirika wa maendeleo, na wadau wote kwa ujumla. Ni matumaini yangu kuwa muhtasari huu utatoa taarifa muhimu kwa wadau kuhusu maendeleo ya sekta ndogo ya umeme nchini.**

..................................................................

Dkt. James A. Mwainyekule
**Mkurugenzi Mkuu**

# VIFUPISHO VYA MANENO

| **EWURA** | **Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji** |
|---|---|
| TANESCO | Shirika la Umeme Tanzania |
| Km | Kilomita |
| MW | Megawati |



# MUHTASARI WA RIPOTI

Ripoti hii inawasilisha utendaji wa kiudhibiti katika sekta ndogo ya umeme kuanzia tarehe 1 Julai 2024 hadi tarehe 30 Juni 2025. Imeandaliwa chini ya Kifungu Na. 30(7) cha sheria ya umeme sura ya 131 kinachoitaka EWURA kutoa taarifa za kiudhibiti zikiwemo zile zinazohusu utendaji wa kampuni zinazodhibitiwa, upatikanaji wa umeme, uwekezaji, ufanisi wa kiutendaji, maendeleo ya umeme, na huduma kwa wateja.

Sekta ndogo ya Umeme ina taasisi mbalimbali zinazochangia katika ukuaji wake. Miongoni mwazo ni Wizara ya Nishati ambayo ndio msimamizi mkuu, EWURA ambayo ina jukumu la udhibiti wa kiufundi na kiuchumi, Wakala ya Nishati Vijijini ambayo ina wajibu wa kusambaza umeme vijijini, na TANESCO ambayo ina wajibu wa kuzalisha, kusafirisha, kusambaza, na kufanya biashara ya umeme ndani na nje ya nchi. Pamoja na na wadau hawa, zipo pia kampuni binafsi ambazo zina wajibu wa kuzalisha na kusambaza umeme.

Katika Kipindi cha mwaka wa fedha wa 2024/2025, kulikuwa na leseni 37 za uzalishaji umeme, kampuni 13 zilizosajiliwa kufanya shughuli za uzalishaji umeme chini ya Megawati 1, leseni 10,367 za wafungaji wa mifumo ya umeme. Pia kulikuwa na leseni moja ya usafirishaji wa umeme pamoja, leseni mbili za usambazaji wa umeme na leseni moja ya kufanya biashara ya umeme nje ya mipaka ya nchi.

Mchakato wa miradi miwili yenye Megawati 200 (MW 100 nguvu ya jua; na MW 100 upepo) uliidhinishwa kutekelezwa kati ya TANESCO na wawekezaji binafsi. Hii inafanya kuwepo kwa miradi sita yenye jumla ya Megawati 936 iliyoidhinishwa ili kuanza kutekelezwa kwa ubia kati ya TANESCO na Sekta Binafsi.

Mikataba 67 ya kuuziana umeme ilikuwa hai, na kulikuwa na kampuni 7 zenye bei elekezi za kuuzia wateja umeme. Pia bei elekezi kwa Kampuni zinazozalisha na kuuza umeme kuanzia Megawati 0.1 hadi 10 kwenye mfumo wa gridi ya taifa na nje ya mfumo huo zilikuwepo.

Uwezo wa kuzalisha umeme uliongezeka kufikia megawati 4,504.54 kutoka megawati 2,411.33 mwaka 2023/2024. Pia, mahitaji ya umeme yaliongezeka kufikia megawati 2,358.54MW kutoka megawati 1,645.23 mwaka 2023/2024. Miundombinu ya kusafirisha umeme imefikia kilometa 8,303.87k kutoka kilometa 7,524 Juni 2024.

Wateja walifikia 5,485,676 kutoka 4,982,259 mwaka 2023/2024. Vilevile, mashauri 104 kati ya watoa huduma na wateja yalitatuliwa. Ukatikaji wa umeme ulitokea mara 17.69 ambapo uko ndani ya kiwango kinachokubalika cha mara 26. Pia muda wa kukatika umeme ulikuwa dakika 1,692.73 zilizokuwa juu ya kiwango cha dakika 1,536 zinazohimilika.

Miradi mbalimbali ipo katika hatua za kukamilika. Uwekezaji katika miradi hiyo unahusisha miradi inayojengwa na serikali ikiwemo miradi mitano ya kuzalisha umeme wa jumla ya megawati 2,235.5, miradi 30 yenye kilomita 15,034.63 za miundombinu ya kusafirisha umeme, na miradi 33 ya vituo vya kupozea umeme vyenye uwezo wa MVA 5,980. Uwekezaji kutokana na sekta binafsi nao uliongezeka, kwa kuwa na miradi 44 ya kuzalisha umeme wa megawati 209.62, ambayo ilikuwa katika hatua mbalimbali za utekelezaji.

Katika kipindi cha mwaka husika, miongoni mwa changamoto zilizojitokeza ni pamoja na kuongezeka kwa matumizi ya umeme kutokana na kuongezeka kwa shughuli za kiuchumi na kijamii zilizochangiwa na ukuaji wa teknolojia hususani kuongezeka kwa magari ya umeme, matumizi bora ya nishati ya kupikia na reli ya umeme.

Kwa ujumla, sekta ndogo ya umeme iliendelea kuimarika. Serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali itaendelea kuweka mazingira mazuri ya uwekezaji ili kuimarisha upatikanaji wa umeme wa uhakika na huduma bora kwa wananchi.

## 1.0 UTANGULIZI

Nishati ya umeme ni kichocheo muhimu sana katika ustawi wa maendeleo ya kiuchumi na kijamii. Kwa sababu hiyo, serikali imeanzisha taasisi mbalimbali kuhakikisha upatikanaji wa umeme kwa viwango vinavyokubalika kwa mujibu wa sheria na miongozo mbalimbali ya nchi.

Miongoni mwa taasisi muhimu katika sekta hiyo ni pamoja na Wizara ya Nishati ambayo ndio msimamizi mkuu, Wakala ya Nishati Vijijini (REA), Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), EWURA ambayo inadhibiti kiufudi na kiuchumi, na wawakezaji binafsi ambao pia wanatoa huduma za umeme.

Sheria ya Umeme kifungu cha 5 kinaipa EWURA jukumu la kiudhibiti katika Sekta ndogo ya Umeme. EWURA inatoa leseni kwa kampuni zinazofanya au zinazotarajia kufanya shughuli zinazodhibitiwa, inatoa bei ya kuuza na kununua umeme, na kuzisimamia bei husika, inasimamia vigezo na masharti vinavyotumika kwa shughuli zinazopewa leseni na pia inaidhinisha kuanza kwa utekelezaji wa miradi ya umeme.


EWURA inatekeleza majukumu yake kwa mujibu wa kifungu cha 6 cha Sheria ya Umeme. Pamoja na mambo mengine, pia inajukumu la kulinda maslahi ya watumia huduma kupitia ushindani, na upatikanaji wa bei stahiki ya umeme. EWURA pia inasimamia uwekezaji wenyegharama stahiki ili kuhakikisha gharama stahiki kwa mtumiaji, usalama wa upatikanaji wa huduma ya umeme, na kusimamia ufanisi kwa kutumia viwango vinavyotambulika.

Ripoti hii inaarifu utendaji katika sekta ndogo ya umeme kwa mwaka wa fedha 2024/2025 kwa taasisi zinazotoa huduma ya umeme nchini, ikiwa ni pamoja na uzalishaji, usafirishaji, usambazaji, na biashara ya umeme nje ya mipaka ya nchi.

Ripoti hii imeandaliwa kwa mujibu wa kifungu cha 30 cha sheria ya umeme, sura 131 ambacho kinaitaka EWURA kufuatilia, kupima na kutoa taarifa kwa umma juu ya utendaji wa taasisi zinazodhibitiwa. Vyanzo vya taarifa zilizotumika katika uandaaji wa ripoti hii ni taasisi husika, na kaguzi mbalimbali za EWURA katika taasisi hizo.

## 2.0 MUUNDO WA SEKTA NDOGO YA UMEME


Sekta ndogo ya umeme inahusisha taasisi mbalimbali na majukumu yake kama zilivyoainishwa kwenye **Kielelezo Na. 1**.





**Kielelezo Na. 1: Taasisi na majukumu yake katika Sekta Ndogo ya Umeme**

# 3.0 LESENI NA USAJILI

Shughuli za uzalishaji, au usafirishaji umeme kuanzia megawati moja (1) na zaidi, zinahitaji kuwa na leseni kwa mujibu wa kifungu Na.8(10 cha sheria ya umeme sura 131. Pia shughuli za namna hiyo zilizo chini ya megawati moja zinahitaji kusajiliwa kwa mujibu wa kifungu namba 18(3). Hadi kufikia Juni 2025, kulikuwa na leseni 10,446 zilizotolewa (**Kielelezo Na. 2**). Kati ya hizo, leseni 1,384 zilitolewa kwa mwaka wa fedha 2024/25, na kampuni 13 zilipewa leseni za uzalishaji wa umeme.




**Kielelezo Na. 2: Leseni zilizotolewa kufika Juni 2025**

## 4.0 VIBALI VYA UJENZI WA VITUO VYA KUZALISHA UMEME

Kufikia Juni 2025, miradi sita ilikuwa imepata vibali vya ujenzi wa vituo vya kuzalishia umeme kwa mujibu wa kifungu cha 5(d) cha sheria ya umeme sura ya 131. Mchanganuo wa miradi hiyo uko kwenye **Kielelezo Na. 3**.

**Kuzalisha Umeme kwa Kutumia Gesi**

(1). Mtambo wa Kinyerezi III. Ukubwa wa megawati 300. Maadalizi ya kuanza ujenzi yanaendelea.

(2). Mtambo wa Somanga Fungu. Ukubwa wa megawati 350. Maandalizi ya kuanza ujenzi yanaendelea.

**Kuzalisha Umeme kwa Kutumia Majilia**

(1). Mtambo wa Masigira. Ukubwa wa megawati 72. Maandalizi ya kuanza ujenzi yanaendelea.

(2). Mtambo wa Kikagati - Murongo. Ukubwa wa megawati 7. Ujenzi umekamilika.

Manunuzi yaliyopata idhini ya ufungaji mitambo ya uzalishaji umeme

**Kuzalisha Umeme kwa Kutumia Jua**

Mtambo wa Kikagati-Murongo wa kuzalisha umeme kwa kutumia maji. Mtambo huo ukubwa wa megawati 14. Mradi umekamilika na unazalisha umeme.

**Kuzalisha Umeme kwa Kutumia Upepo**

Mtambo wa Somanga Fungu wa kuzalisha umeme kwa kutumia gesi. Mtambo huu una ukubwa wa megawati 350. Maadalizi ya kuanza ujeniz yanaendelea.

**Kielelezo Na. 3: Ujenzi wa vituo vya kuzalisha umeme kufikia Juni 2025**

## 5.0 MIKATABA YA KUUZIANA UMEME

Kufika Juni 2025, mikataba 67 ya kuuziana umeme wa jumla ya megawati 698.72 ilikuwa imeidhinishwa kwa mujibu wa kifungu cha 25(3) cha sheria ya umeme sura ya 131, (**Kielelezo Na. 4**). Mikataba hiyo ilisainiwa kati ya TANESCO na kampuni binafsi za kuzalisha umeme za ndani na nje ya nchi. Ujenzi wa mitambo kwenye mikataba 23 kati ya hiyo umekamilika na kuchangia Megawati 489.10. Mikataba mingine 8 yenye jumla ya Megawati 36.23, miradi yake iko katika hatua za ujenzi, mikataba 36 yenye Megawati 173.39 miradi iko katika hatua za kuanza ujenzi.

Mikataba 64 (megawati 641.72) Kati ya TANESCO na kampuni za kuzalisha umeme nchini + Mikataba mitatu (Megawati 57.00) kati ya TANESCO na Kampuni za kuzalisha umeme nje ya nchi = Mikataba 67 (Megawati 698.72) kati ya TANESCO na Kampuni za ndani na nje ya nchi

**Kielelezo Na. 4: Mikataba ya Kuuziana Umeme, kufikia Juni 2025**

## 6.0 BEI ZA KUUZA UMEME


Kufikia Juni 2025, makundi mbalimbali ya wazalishaji umeme yalikuwa yameidhinishiwa bei za umeme kwa mujibu wa kifungu cha 5(b) cha sheria ya umeme sura ya 131, (**Kielelezo Na. 5**). Miongoni mwa bei hizo, ni zile za kuuza umeme kwa wateja na ambazo zilitolewa kwa kampuni saba (7) ikiwemo TANESCO na bei za kampuni binafsi kuuza umeme kwa TANESCO kwa mitambo yote yenye uwezo chini ya megawati moja.




**Kielelezo Na. 5: Bei za Kuuza Umeme Kufikia Juni 2025**

## 7.0 MALALAMIKO NA USULUHISHI

Usuluhishi wa malalamiko ya wateja dhidi ya watoa huduma wao ulifanyika kwa mafanikio na kwa mujibu wa sheria, ambapo malalamiko 104 kati ya TANESCO na wateja wake yalisuluhishwa katika kipindi cha mapitio ya ripoti hii (**Kielelezo Na. 6**).





**Kielelezo Na. 6: Usuluhishi wa Malalamiko kwa Mwaka wa Fedha 2024/25**

# 8.0 UZALISHAJI WA UMEME

Taarifa za uzalishaji wa umeme huzingatia vigezo mbalimbali, kama vile uwezo wa mitambo, mahitaji ya umeme, mgawanyiko wa uzalishaji wa umeme, uzalishaji na uingizaji umeme toka nchi jirani na ushiriki wa kampuni binafsi.

## 8.1 Uwezo wa mitambo ya kuzalisha umeme

Kufikia Juni 2025, uwezo wa mitambo kuzalisha umeme ulikuwa megawati 4,504.54 (**Kielelezo Na. 7**), ambapo TANESCO ilichangia kwa asilimia 85.12 (**Kielelezo Na. 8**).




| | 2017/18 | 2018/19 | 2019/20 | 2020/21 | 2021/22 | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 | 2025/26 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Jumla | 1,742.95 | 1,833.61 | 1,792.12 | 1,906.67 | 2,044.85 | 2,249.39 | 2,670.62 | 4,504.54 | 4,504.54 |
| Gridi ya Taifa | 1,461.06 | 1,565.72 | 1,565.72 | 1,574.45 | 1,694.55 | 1,874.34 | 2,373.00 | 3,997.07 | 3,997.07 |
| Nje ya Gridi ya Taifa | 57.14 | 35.95 | 36.08 | 34.80 | 45.88 | 37.12 | 38.00 | 78.37 | 78.37 |
| Matumizi Binafsi | 189.75 | 196.94 | 155.32 | 262.42 | 262.42 | 295.92 | 195.62 | 362.10 | 362.10 |
| Kutoka nje ya Nchi | 35.00 | 35.00 | 35.00 | 35.00 | 42.00 | 42.00 | 64.00 | 67.00 | 67.00 |

**Kielelezo Na. 7: Uwezo wa mitambo Kuzalisha Umeme Kufikia Juni 2025**


**UWEZO WA KUZALISHA UMEME KWA MWAKA WA FEDHA 2024/25**

| Kampuni | Uwezo (Megawati) | Mchango (%) | |
|---|---|---|---|
| TANESCO | 3,834.44 | 85.12% | 100.00% |
| Wazalishaji Wakubwa wa Umeme (≥10 Megawati) | 189.00 | 4.20% | |
| Wazalishaji Wadogo wa Umeme ((>0.1 Megawati& ≤10 Megawati ) | 49.79 | 1.11% | |
| Wazalishaji Wadogo Zaidi wa Umeme (≥0.15 Megawati & ≤0.1MW) | 2.77 | 0.06% | |
| Matumizi Binafsi | 361.53 | 8.03% | |
| Kutoka nje yaMioaka ya Nchi | 67.00 | 1.49% | |
| **Total** | **4,504.54** | **100.00%** | |

**Kielelezo Na. 8: Mchango katika Mitambo ya Kuzalisha Umeme – Mwaka 2024/2025**

## 8.2 Mahitaji ya Umeme

Mahitaji ya umeme nchini yameendelea kuongezeka, kutokana na kukua kwa shughuli za kiuchumi na kijamiii. Kufikia Juni 2025, mahitaji ya umeme katika gridi ya taifa yalikuwa yamefikia megawati 2,358.54 (**Kielelezo Na. 9**).




| | 2017/18 | 2018/19 | 2019/20 | 2020/21 | 2021/22 | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Nje ya Grid ya Taifa | 30.00 | 31.00 | 36.00 | 45.00 | 51.00 | 57.00 | 66.00 | 75.00 |
| Matumizi Binafsi | 189.75 | 196.94 | 155.32 | 262.42 | 262.42 | 295.92 | 195.62 | 362.10 |
| Grid ya Taifa | 1,045.70 | 1,116.58 | 1,151.66 | 1,201.02 | 1,340.68 | 1,470.50 | 1,645.23 | 1,921.44 |
| Jumla | 1,265.45 | 1,344.52 | 1,342.98 | 1,508.44 | 1,654.10 | 1,823.42 | 1,906.85 | 2,358.54 |

**Kielelezo Na. 9: Mahitaji ya Umeme Kufikia Juni 2025**

## 8.3 Mgawanyiko Wa Uzalishaji Wa Umeme

Uzalishaji wa Umeme ulichangiwa na mitambo ya maji, gesi, mafuta, tungamo taka, jua na upepo. Maji yalichangia kwa asilimia 64.77, Gesi Asilia asilimia 34.68, mafuta kwa asilimia 0.24, tungamo taka kwa asilimia 0.26, Upepo asilimia 0.03, na Jua asilimia 0.02 (**Kielelezo Na. 10**).




| | 2017/18 | 2018/19 | 2019/20 | 2020/21 | 2021/22 | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Upepo | 0.00% | 0.00% | 0.00% | 0.00% | 0.00% | 0.00% | 0.00% | 0.03% |
| Jua | 0.00% | 0.00% | 0.00% | 0.00% | 0.00% | 0.00% | 0.00% | 0.02% |
| Tungamo Taka | 0.23% | 0.20% | 0.20% | 0.18% | 0.00% | 0.12% | 0.01% | 0.26% |
| Mafuta | 3.75% | 0.10% | 0.00% | 0.15% | 0.19% | 0.14% | 0.47% | 0.24% |
| Gesi | 64.11% | 67.50% | 62.41% | 60.55% | 68.32% | 72.82% | 67.10% | 34.68% |
| Maji | 31.89% | 32.30% | 37.39% | 39.12% | 31.49% | 26.92% | 32.42% | 64.77% |

**Kielelezo Na. 10: Mgawanyiko wa uzalishaji umeme kufikia Juni 2024**

## 8.4 Uzalishaji Na Uingizaji Umeme Toka Nchi Jirani

Kiwango cha uzalishaji umeme nchini na kutoka nchi za jirani kiliendelea kuongezeka hadi kufikia GWh 13,940.06 kufikia Juni 2025 (**Kielelezo Na. 11**). TANESCO ilichangia GWh 12,437.99 sawa na asilimia 89.22 ya umeme wote uliozalishwa na ule wa kutoka nchi jirani (Kielelezo Na. 12).




| | 2017/18 | 2018/19 | 2019/20 | 2020/21 | 2021/22 | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Jumla | 7,490.93 | 7,963.67 | 8,081.46 | 8,674.80 | 9,647.47 | 10,425.38 | 11,438.99 | 13,940.06 |
| Grid ya taifa | 6,833.85 | 7,372.88 | 7,602.45 | 7,973.30 | 8,912.19 | 9,606.56 | 10,704.46 | 12,514.55 |
| Nje ya Grid ya Taifa | 183.91 | 96.58 | 75.13 | 78.86 | 87.51 | 84.44 | 99.65 | 260.15 |
| Mayumizi Bonafsi | 359.46 | 373.08 | 294.25 | 497.14 | 497.14 | 560.60 | 370.59 | 872.51 |
| Kutoka Nje ya Nchi | 113.71 | 121.13 | 109.63 | 125.50 | 150.63 | 173.78 | 264.29 | 292.85 |

**Kielelezo Na. 11: Uzalishaji wa umeme kufikia Juni 2025**

| UZALISHAJI UMEME NCHINI NA UINGIZAJI UMEME TOKA NJE YA NCHI MWAKA WA FEDHA 2024/25 | | | |
|---|---|---|---|
| ufafanuzi | Kampuni | Umeme ("GWh") | Mchango(%) |
| Total | TANESCO | 12,423.85 | 89.12% |
| | Wazalishaji Wakubwa wa Umeme (≥10 Megawati) | 246.50 | 1.77% |
| | Wazalishaji Wadogo wa Umeme ((>0.1 Megawati& ≤10 Megawati ) | 99.91 | 0.72% |
| | Wazalishaji Wadogo Zaidi wa Umeme (≥0.15 Megawati & ≤0.1MW) | 5.58 | 0.04% |
| | Matumizi Binafsi | 871.37 | 6.25% |
| | Kutoka nje yaMioaka ya Nchi | 292.85 | 2.10% |
| | **Jumla** | **13,940.06** | **100.00%** |


**Kielelezo Na. 12: Mgawanyiko wa uzalishaji Umeme - 2024/2025**

# 9.0 USAFIRISHAJI UMEME

Taarifa juu ya usafirishaji wa umeme ilizingatia vigezo mbalimbali. Miongoni mwa vigezo hivyo ni miundombinu husika, ufanisi wake, na wateja.

## 9.1 Miundombinu

Kufikia Juni 2025, urefu wa miundombinu ya kusafirishia umeme ilifikia kilometa 8,303.87. Vilevile, uwezo wa vituo vya kupoozea umeme ulifikia MVA 10,477.40 *(***Kielelezo Na. 13***).*




**Kielelezo Na. 13: Uwezo wa Miundombinu ya Njia za Kusafirisha Umeme**

## 9.2 Wateja


Kufikia Juni 2025, wateja wakubwa saba walikuwa wameunganishwa kwenye miundombinu ya usafirishaji (**Kielelezo Na. 14**). Wateja hao wameunganishwa katika msongo wa kilovoti 220 na 132.

| Wateja Walionganishwa na Miundombinu ya Usafirishaji | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Mgodi wa Dhahabu wa Bulyanhulu ( 220kV) | Shirika la Umeme Zanzibar (132kV) | Kiwanda cha Simenti cha Tanganyika Portland (132kV) | kiwanda cha Simenti cha Tanga (132kV) | Kiwanda cha simenti cha Rhino (132kV) | Mgodi wa Dhahabu wa Nyamongo (132kV) | Mgodi wa Dhahabu wa Buzwagi (132kV) |

**Kielelezo Na. 14: Wateja kwenye miundombinu ya kusafirisha umeme kufikia Juni 2025**

## 9.3 Ufanisi Wa Miundombinu

Ufanisi wa miundombinu ya usafirishaji umeme uliendelea kuimarika (**Kielelezo Na. 15**). Kwa mwaka 2024/25, kiwango cha upatikanaji umeme kilikuwa mara 6.4, chini ya kikomo cha mara 10, wakati ambapo masaa ya ukatikaji umeme yalikuwa 4.6, ambayo ni chini ya kikomo cha masaa 6.5.





**Kielelezo Na. 15: Ufanisi wa Miundombinu ya Usafirishaji kufikia Juni 2025**

# 10.0 USAMBAZAJI UMEME

Taarifa juu ya usafirishaji wa umeme ilizingatia vigezo mbalimbali. Miongoni mwa vigezo vilivyozingatiwa ni miundombinu, wateja na ufanisi wa miundombinu.

## 10.1 Miundombinu

Miundombinu ya usambazaji wa umeme iliendelea kuongezeka. Kufikia Juni 2025, urefu wa miundombinu hiyo ulifikia kilomita 214,343.67. Kampuni zenye leseni (TANESCO na Mwenga) zilikuwa na miundombinu yenye urefu wa kilometa 213,726.82 (**Kielelezo Na. 16**). Kampuni zilizosajiliwa zilikuwa na miundombinu yenye urefu wa kilometa 617. Ongezeko hili limewezesha Watanzania wengi zaidi kupata huduma ya umeme iliyo bora na uhakika.





| | 2017/18 | 2018/19 | 2019/20 | 2020/21 | 2021/22 | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Total | 103,640.36 | 109,639.60 | 139,978.21 | 149,579.64 | 161,407.47 | 164,361.41 | 188,883.08 | 214,343.67 |
| TANESCO | 103,289.36 | 109,225.60 | 139,092.86 | 148,544.23 | 160,366.86 | 163,296.06 | 187,817.73 | 213,278.32 |
| Mwenga | 351.00 | 414.00 | 437.00 | 439.00 | 444.00 | 448.50 | 448.50 | 448.50 |
| Powercorner | - | - | 152.00 | 152.00 | 152.00 | 152.00 | 152.00 | 152.00 |
| Jumeme | - | - | 104.70 | 215.47 | 215.47 | 247.12 | 247.12 | 247.12 |
| PowerGen | - | - | 112.90 | 150.19 | 150.19 | 150.19 | 150.19 | 150.19 |
| EON | - | - | 46.20 | 46.20 | 46.20 | - | - | - |
| Watu na Umeme | - | - | 7.75 | 7.75 | 7.75 | 7.75 | 7.75 | 7.75 |
| Andoya | - | - | 24.80 | 24.80 | 25.00 | 59.79 | 59.79 | 59.79 |

**Kielelezo Na. 16: Urefu wa Miundombinu ya kusambaza umeme**

## 10.2 Wateja

Idadi ya wateja waliounganishiwa umeme iliendelea kuongezeka (**Kielelezo Na. 17**). Kufikia Juni 2025, idadi ya wateja ilikuwa 5,485,676. Kati ya hao, TANESCO ina wateja 5,460,695 sawa na asilimia 99.5%.





| | 2017/18 | 2018/19 | 2019/20 | 2020/21 | 2021/22 | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Total | 2,226,559 | 2,488,158 | 2,879,945 | 3,312,705 | 3,864,827 | 4,422,940 | 4,982,259 | 5,485,676 |
| TANESCO | 2,223,638 | 2,484,202 | 2,864,560 | 3,290,490 | 3,842,096 | 4,400,070 | 4,957,278 | 5,460,695 |
| Mwenga | 2,921 | 3,956 | 4,591 | 5,105 | 5,621 | 5,636 | 7,269 | 7,269 |
| Powercorner | - | - | 3,011 | 3,013 | 3,013 | 3,013 | 3,013 | 3,013 |
| Jumeme | - | - | 4,874 | 9,860 | 9,860 | 10,460 | 10,938 | 10,938 |
| PowerGen | - | - | 2,177 | 3,227 | 3,227 | 3,227 | 3,227 | 3,227 |
| EON | - | - | 476 | 476 | 476 | - | - | - |
| Watu na Umeme | - | - | 256 | 256 | 256 | 256 | 256 | 256 |
| Andoya | - | - | - | 278 | 278 | 278 | 278 | 278 |

**Kielelezo Na. 17: Idadi ya Wateja**


## 10.3 Ufanisi Wa Miundombinu

Ufanisi wa miundombinu ya usambazaji umeme uliendelea kuimarika. Katika kipindi cha marejeo, wastani wa ukatikaji wa umeme ulikuwa mara 17.69 ambao ni chini ya kikomo cha mara 26 (**Kielelezo Na. 18**). Wastani wa dakika ya ukatikaji umeme zilikuwa dakika 1,692.73 ambazo ni juu ya kikomo cha dakika 1,536 (**Kielelezo Na. 19**).




| | 2018/19 | 2019/20 | 2020/21 | 2021/22 | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 | KIPIMO |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| TANESCO | 46.03 | 218.00 | 48.00 | 11.00 | 26.00 | 13.59 | 17.69 | 26.00 |
| MWENGA | 19.10 | 35.93 | 28.00 | 14.00 | 30.00 | 17.73 | 17.73 | 26.00 |
| ANDOYA | 124.00 | 1.00 | 1.00 | 193.00 | 97.00 | 95.00 | 95.00 | 26.00 |

**Kielelezo Na. 18: Wastani wa idadi ya ukatikaji umeme**





| | 2018/19 | 2019/20 | 2020/21 | 2021/22 | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 | KIPIMO |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| TANESCO | 2,784 | 10,560 | 22,380 | 26,820 | 1,536 | 554 | 1,693 | 1,536 |
| MWENGA | 803 | 1,570 | 1,848 | 1,380 | 1,737 | 844 | 844 | 1,536 |
| ANDOYA | 255 | 66 | 8 | 328 | 102 | 101 | 101 | 1,536 |

**Kielelezo Na. 19: Wastani wa Dakika za Ukatikaji Umeme**

# 11.0 UPOTEVU WA UMEME

Kiwango cha upotevu wa umeme kiliendelea kupungua katika kipindi cha marejeo (**Kielelezo Na. 20**). Kwa mwaka 2024/25, upotevu wa umeme katika miundombinu ya kusafirishia ulipungua hadi kufikia asilimia 5.86, wakati ambapo kwa miundombinu ya usambazaji umeme ilikuwa asilimia 8.29.




| | 2017/18 | 2018/19 | 2019/20 | 2020/21 | 2021/22 | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 | KIKOMO | Target |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| TANESCO-Usambazaji Umeme | 4.53 | 10.35 | 9.41 | 9.50 | 8.75 | 8.69 | 8.75 | 8.00 | 9.00 | 9.00 |
| TANESCO-Usafirishaji Umeme | 5.89 | 5.87 | 5.89 | 5.89 | 5.89 | 5.88 | 5.86 | 5.86 | 5.88 | 5.88 |
| TANESCO-Usafirishaji na Usambazaji Umeme | 10.42 | 16.22 | 15.30 | 15.39 | 14.64 | 14.57 | 14.61 | 13.86 | 14.88 | 14.88 |
| MWENGA-Usambazaji Umeme | 3.69 | 4.24 | 4.73 | 5.49 | 6.00 | 5.99 | 6.00 | 6.00 | 9.00 | 9.00 |
| ANDOYA-Usambazaji Umeme | 7.41 | 5.75 | 5.59 | 4.34 | 3.98 | 1.33 | 1.31 | 1.31 | 9.00 | 9.00 |


**Kielelezo Na. 20: Upotevu wa Umeme**

# 12.0 UWEKEZAJI KWENYE MIUNDOMBINU YA UMEME

Uwekezaji katika sekta ndogo ya umeme uliendelea kuimarika. Miradi mbalimbali ya uzalishaji na usafirishaji umeme iliendelea kutekelezwa, kama inavyoelezwa katika sehemu inayofuata.

## 12.1 Uwekezaji katika miundombinu ya kuzalisha umeme

Serikali inatekeleza miradi mitano ya kimkakati ambayo iko katika hatua mbali mbali (**Kielelezo Na. 21**). Miradi hiyo itakuwa na uwezo wa kuzalisha megawati 2,420.50 pindi itakapokamilika.




**Kielelezo Na. 21: Maendeleo ya Miradi ya Kuzalisha Umeme kufikia Juni 2025**

## 12.2 Uwekezaji Katika Miundombinu ya Kusafirisha Umeme

Serikali inatekeleza miradi 30 ya njia za kusafirisha umeme zenye urefu wa kilometa 5,034.63, ikiwa katika hatua mbalimbali (**Kielelezo Na. 22**). Vilevile, miradi 33 ya vituo vya kupooza umeme yenye uwezo wa MVA 5,980.00 ilikuwa katika hatua mbalimbali za utekelezaji (**Kielelezo Na. 23**).

| Na. | Maelezo | Idadi | Urefu ("km") |
|---|---|---|---|
| 1 | Miradi Iliyokamilika | 10 | 1,841.80 |
| 2 | Miradi Inayoendelea | 20 | 3,192.83 |
| 3 | Jumla | 30 | 5,034.63 |

**Kielelezo Na. 22: Maendeleo ya Miradi ya Njia za Kusafirisha Umeme**

| Na. | Maelezo | Idadi | Uwezo ("MVA") |
|---|---|---|---|
| 1 | Miradi Iliyokamilika | 6 | 365.00 |
| 2 | Miradi Inayoendelea | 27 | 5,615.00 |
| 3 | Jumla | 33 | 5,980.00 |

**Kielelezo Na. 23: Maendeleo ya Miradi ya Vituo Vya Kupoza Umeme kufikia Juni 2025**

## 12.3 Ushiriki wa wawakezaji binafsi katika miundombinu ya umeme


Miradi binafsi 67 iko katika hatua mbalimbali za utekelezaji (**Kielelezo Na. 24**). Miradi hiyo itakuwa na uwezo wa kuzalisha umeme wa megawati 698.72.

| Na. | Melezo | Idadi | Uwezo ("MW") |
|---|---|---|---|
| 1 | Miradi Iliyokamilika | 23 | 489.10 |
| 2 | Miradi Iliyokatika Ujenzi | 8 | 36.23 |
| 3 | Miradi Iliyokatika hatua za kuanza ujenzi | 36 | 173.39 |
| | **Total** | **67** | **698.72** |

**Kielelezo Na. 24: Ushiriki wa Kampuni Binafsi Katika Uwekezaji Hadi Kufikia Juni 2025**

## 13.0 NISHATI SAFI YA KUPIKIA


Mkakati wa Nishati Safi ya Kupikia wa Mwaka 2024 unalenga kuhakikisha kuwa asilimia 80 ya kaya zote nchini zinatumia nishati safi ya kupikia kufikia mwaka 2034. Takwimu zinaonesha kuwa hadi kufikia mwaka 2021, asilimia 6.9 tu ya kaya ndio zilikuwa zikitumia nishati safi kupikia (**Kielelezo Na. 25**). Serikali itaendelea kuweka mazingira mazuri ya kufikia lengo hilo, ikiwemo kuweka mifumo thabiti ya kiudhibiti ya kuvutia matumizi ya nishati safi, upatikanaji wa umeme, upatikanaji wa vifaa nafuu vya kupikia vinavyotumia umeme, na uhamasishaji wa wananchi.




**Kielelezo Na. 25: Kaya Zenye Nishati Safi ya Kupikia Kufika Mwaka 2021**

## 14.0 TATHMINI YA USHINDANI KATIKA SOKO

Ushidani katika soko unaonyesha kuwa TANESCO inamiliki asilimia 85.12 ya mitambo ya kuzalisha umeme (**Kielelezo Na. 26**). Hii inaonyesha uhitaji mkubwa uliopo wa ongezeko la wawekezaji wa Sekta binafsi.




**Kielelezo Na. 26: Ushindani wa Soko katika Kuzalisha Umeme Kufika Juni 2025**

# 15.0 MATOKEO YA UDHIBITI

Udhibiti umechangia sehemu kubwa ya maendeleo ya sekta ndogo ya umeme, kiuchumi, na kijamii kwa ujumla. Miongoni mwa matokeo ya udhibiti ni kama ifuatavyo:

## 1). Uwezo wa Kumudu Gharama za Umeme

Leseni 1,371 za ufungaji wa mifumo ya meme na gharama za mauziano ya umeme zillidhinishwa kwa Kampuni saba (7) zinazouza meme kwa wateja, na zilichangia kuimarisha ushindani katika soko na kudhibiti bei za meme, hivyo kusaidia uwepo wa aharama zinazohimilika.

## 2). Uhakika wa Upatikanaji Umeme

Leseni 13 za kuzalisha umeme megawati 160.86 pamoja na mikataba 14 ya kuuziana meme wa megawati 258.71 itachangia katika uhakika wa upatikanaji umeme pindi itakapokamilika.

## 3). Uhakika na Ubora wa Umeme

Uwepo wa makubaliano ya mikataba ya utendaji pamoja na ukaguzi wa mara kwamara kwa kampuni zinazodhibitiwa, umechangia kuimarika kwa uhakika na ubora wa umeme.

### 4). Uwekezaji

Mazingira mazuri ya uwekezaji pamoja na mifumo mizuri ya kiudhibiti, vimechangia serikali kuwekeza katika miradi mitano ya kuzalisha umeme (Megawati 2,420.50), miradi 30 ya njia za kusafirisha umeme (kilometa 5,034.63), vituo 33 vya kupoza umeme (MVA 5,980) na uwekezaji wa kampuni binafsi katika miradi 44 ya kuzalisha umeme wa megawati 209.62.

### 5). Ustawi wa Kampuni Zinazodhibitiwa

Vidhinishwaji gharama za uuzaji umeme kwa kampuni sita (6) umechangia kuhakikisha mapato stahiki kwa uwekezaji na hivyo kuchangia kustawi kwa kampuni hizo.

### 6). Usambazaji Umeme

Mafanikio yaliyopatikana katika kuidhinisha leseni, bei za umeme, na mikataba ya mauziano ya meme, yalichangia kuunganishwa meme kwa wateja wapya 503.417.

## 16.0 USIMAMIZI WA MASLAHI YA WATEJA

Katika kusimamia maslahi ya wateja wa huduma zinazodhibitiwa, hatua mbalimbali zilichukuliwa. Miongoni mwa hatua hizo ni:

### 1). Mkataba wa Huduma kwa Wateja

Ukaguzi wa mara kwa mara ulifanyika kwa kampuni zote ili kuhakikisha kuwa zinati makubaliano yaliyomo kwenye mikataba ya huduma kwa wateja. Hi ilisaidia utendaji kufika asilimia 82 na hivyo kuchangia katika kuimarika kwa huduma kwa wateja.

### 2). Ukaguzi wa Utendaji

Ukaguzi wa mara kwa mara ulifanyika kwa kampuni zote ili kuhakikisha kuwa zinatii miongozo ya kisheria na taratibu mbalimbali za kiudhibiti katika utoaji wa huduma kwa wateja. Ukaguzi ulifanyika katika mikoa yote nchini na kwa kampuni zote zinazodhibitiwa.

## 17.0 MUONEKANO WA SEKTA NDOGO YA UMEME KATIKA MIAKA IJAYO

Sekta ndogo ya umeme inaendelea kukua kutokana na kuwa na mchango mkubwa kiuchumi na kijamii. Muonekano wa sekta ndogo ya umeme katika miaka ijayo unatarajiwa kuwa kama ifuatavyo:

### 1). Mahitaji ya Umeme

Mahitaji ya meme yanakadiriwa kuendelea kukua hadi kufikia GWh 16,007.5 ifikapo 2030. Pia kunatarajiwa kuongezeka utumiaji wa meme kwa kila mtu kutoka kWh 243 mwaka 2025 hadi kufikia kWh 528 mwaka 2030, huku idadi ya wateja waliounganishwa na huduma ya umeme ikipanda kutoka asilimia 50 mwaka 2025 hadi asilimia 87 mwaka 2030.

### 2). Uzalishaji Umeme

Kutokana na kuongezeka kwa mahitaji ya umeme, uzalishaji wake unatarajiwa kuongezeka pia. Uzalishaji wa umeme unakadiriwa kuongezeka hadi kufikia megawati 19,905.19 mwaka 2050.

## 18.0 MAFANIKIO

Sekta ndogo ya umeme imekuwa na mafanikio kadhaa katika mwaka 2023/2024. Miongoni mwa mafanikio hayo ni kama ifuatavyo:

### 1). Leseni za Kuzalisha Umeme

Leseni tatu (3) za kuzalisha umeme wa megawati 14.5 ziliidhinishwa a zitachangia katika uhakika wa upatikanaji meme pindi uzalishaji utakapoanza.

### 2). Leseni za Uzalishaji na Ufungaji Mifumo ya Umeme

Leseni 13 za uzalishaji umeme zenye uwezo wa Megawati 160.8 zilitolewa baada ya miradi kukamilika. Pia, leseni 1,371 za ufungaji wa mifumo ya meme zilitolewa kwa watu binafsi ili kuchochea ufungaji bora wa mifumo ya meme na hivyo kuchangia katika usambazaji wa umeme.

## 3). Mikataba ya Kuuziana Umeme

Mikataba 14 ya kuuza meme wa megawati 258.71 ilidhinishwa. Mikataba hiyo itachangia katika upatikanaji wa meme wa uhakika pindi itakapokamilika.

## 4). Ukaguzi wa Miundomninu ya Umeme

Ukaguzi ulifanyika kuhakikisha ufanisi wa utendaji kwa kampuni zote zinazodhibitiwa nchini. Hi ilichangia katika kuimarika kwa upatikanaji wa huduma bora wa umeme.

## 5). Uunganishaji Umeme kwa Wananchi

Wananchi wapatao 5,485,676 walikuwa wameunganishwa a huduma ya umeme katika Mwaka wa Fedha 2024/25, sawa na ongezeko la 503,417 (10.10%) kutoka 4,982,259 katika Mwaka wa Fedha 2023/24.

## 6). Ukaguzi wa Bei za Kuuza Umeme

Ukaguzi Ulifanyika kuhakikisha kuwa meme unauzwa kwa wateja kwa mujibu wa bei za meme zilizoidhinishwa. Hi inahusisha kampuni saba (7) zinazodhibitiwa ikiwemo TANESCO.

## 7). Usuluhishi wa malalamiko

Malalamiko 104 baina ya wateja na watoa huduma yalisuluhishwa na kufikia muafaka na hivyo kuchangia katika mahusiano mema na kuwalinda wateja na watoa huduma katika haki zao.

## 8). Ongezeko la Uwezo wa Kuzalisha Umeme

Uwezo wa kuzalisha umeme uliongezeka kwa megawati 1,833.91 sawa na asilimia 68.67. Ongezeko hilo lilitoka megawati 2,411.33 Mwaka wa Fedha 2023/24 hadi kufika 4,504.54 Mwaka wa Fedha 2024/25.

## 9). Ongezeko la Mahitaji ya Umeme

Mahitaji ya Umeme yaliongezeka kwa megawati 451.68 sawa na asilimia 23.69 Mahitaji yalitoka megawati 1,906.85 Mwaka wa Fedha 2023/24 had 2,358.54 Mwaka wa Fedha 2024/25.

## 10). Ongezeko la Uzalishaji Umeme

Uzalishaji wa Umeme umeongezeka kwa GWh 2,501.07 sawa na asilimia 21.86 kutoka GWh 11,438.99 Mwaka wa Fedha 2023/24 had kufikia GWh 13,940.06 Mwaka wa Fedha 2024/25.

## 11). Ongezeko la Miundombinu ya Laini ya Usafirishaji Umeme

Miundombinu ya Usafirishaji Umeme iliongezeka kwa kilometa 779, sawa na asilimia 10.35. Ongezeko hilo lilitoka kilometa 7,524 Mwaka wa Fedha 2023/24 hadi 8,303.87 Mwaka wa Fedha 2024/25.

## 12). Ongezeko la Vituo vya Kupoza Umeme

Vituo vya kupoza umeme vilikuwa 72, sawa na ongezeko la vituo 5 au asilimia 7.46

## 13). Ongezeko la Miundombinu ya Kusambaza Umeme

Miundombinu ya usambazaji meme iliongezeka kwa kilometa 26,077.44 sawa na asilimia 13.85. Ongezeko hilo lilitoka kilometa 188,266.23 Mwaka wa Fedha 2023/24 hadi kilometa 214,343.67 Mwaka wa Fedha 2024/25.

## 14). Ongezeko la Wateja wa Umeme

Wateja waliongezeka kufikia 5,485,676 Mwaka wa Fedha 2024/25 kutoka 4,982,259 Mwaka wa Fedha 2023/2024. Ongezeko hili ni sawa a wateja 559,595, au asilimia 12.7.

## 15). Kuongezeka kwa Upatikanaji Umeme

Ufanisi katika upatikanaji wa huduma ya meme uliongezeka ambapo kukatika kwa umeme kulikuwa mara 17.69, ikiwa ndani ya kiwango cha chini cha mara 26.

### 16). Kuongezeka kwa uwekezaji

Uwekezaji uliongezeka katika miundombinu ya umeme. Serikali iliwekeza kwenye miradi mitano yenye uwezo wa kuzalisha megawati 2,235.5 ambayo likuwa katika hatua mbalimbali za utekelezaji. Serikali pa iliwekeza katika miradi 30 ya laini za kusafirisha umeme sawa na kilometa 5,034.63. Vile vile serikali iliwekeza kwenye vituo 33 vya kupozea meme, vyenye uwezo wa MVA 5,980.00. Kampuni binafsi ziliwekeza.

### 17). Uhamasishaji wa Nishati Safi ya Kupikia

Uhamasishaji wa nishati safi ya kupikia ulifanyika maeneo mbalimbali ya nchi ili kuhakikisha asilimia 80 ya kaya zote nchini zinatumia nishati safi ya kupikia kufika mwaka 2034. EWURA itaendelea kuweka mazingira mazuri ya kiudhibiti kuwezesha kufikia lengo.

## 19.0 CHANGAMOTO

Changamoto kadhaa zilijitokeza katika kipindi cha mwaka wa fedha 2024/25. Miongoni mwa changamoto hizo ni kama ifuatavyo:

### 1). Ukame katika Mabwawa ya Kuzalisha Umeme

Upungufu wa mvua, uliathiri upatikanaji wa maji katika mabwawa ya kuzalisha umeme. Hata hivyo serikali iliikabili changamoto hiyo kwa kuzalisha meme kupitia vyanzo mbadala ikiwemo gesi asilia.

### 2). Kuongezeka kwa matumizi ya umeme

Kuongezeka kwa matumizi ya meme kutokana kuongezeka kwa shughuli za kiuchumi na kijamil. Miongoni mwa matumizi hayo ni kuanza kwa treni na magari ya umeme, na kupika kwa kutumia nishati ya umeme.

### 3). Ushiriki wa Sekta Binafsi

Ushiriki wa sekta binafsi kwenye uzalishaji kuwa asilimia 17 ni ushiriki ambao bado uko kiwango cha chini.

ewura

Energy and Water Utilities Regulatory Authority

ISO 9001:2015 Certified

MAMLAKA YA UDHIBITI WA
HUDUMA ZA NISHATI NA MAJI
Jengo la EWURA, Mtaa wa EWURA
3 Mtaa wa EWURA,
4114 Tambukareli,
S.L.P. 2857, Dodoma,
Simu: +255 26 2329002-4,
Nukushi: +255 26 2329005,
Barua pepe: info@ewura.go.tz

Tovuti https://www.ewura.go.tz

Huduma kwa Wateja: 0800110030

ewuratanzania ewuratanzania ewuratanzania EWURA TV